



DSE
Creating Opportunities

2018 TAARIFA YA FEDHA YA MWAKA



| Yaliyomo

Page No

Ujumbe wa Mwenyekiti wa Bodi	1 – 3
Ujumbe wa Afisa Mtendaji Mkuu	5 – 7
Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi	9 - 16

Ujumbe wa Mwenyekiti wa Bodi

Utangulizi

Ninayo furaha kubwa kupata fursa hii ya kuwasilisha taarifa ya utendaji na matokeo yake kwa mwaka wa fedha 2018, ikiwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa miaka mitano ya Mpango Mkakati wa DSE (2018 - 2022). Mwaka huu wa fedha, kwa wastani umekuwa mwaka mzuri kwa DSE, kwa kuangalia matokeo ya utendaji kifedha na shughuli za uendeshaji soko. Tumeweza kupata maendeleo mazuri katika utekelezaji wa mpango mkakati wetu wa miaka mitano. Kwa hivyo, nina ari kubwa ya kuwasilisha ripoti ya Mwaka na Taarifa za Fedha za DSE kwa mwaka ulioishia Disemba, 31 2018.

Mazingira ya jumla ya uchumi mkubwa katika Nchi

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), katika kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha wa 2018, kwa wastani, Pato la Taifa (GDP) lilikua kwa asilimia 6.7. Ukuaji wa Pato la Taifa umechangiwa na uwekezaji katika miundombinu, kuuza nje ya bidhaa za asili, hali nzuri ya hewa, ambayo imechangia kuongezeka uzalishaji wa mazao kilimo, n.k. Uwekezaji katika miundombinu na pamoja na ujenzi wa Reli ya kisasa ya umeme (Standard Gauge Railway - SGR), upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam, Utanuzi na ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere, uboreshaji wa mtandandao wa barabara kwa ajili ya maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa kikubwa cha uzalishaji umeme wa maji (Stigler's Gauge Hydropower Plant Station).

Mfumuko wa bei ulibaki kuwa kwenye tarakimu moja, hii ni kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani, kushuka kwa bei za bidhaa kimataifa, hasa kwa bei za mafuta, na utekelezaji wa sera ya kubana matumizi (Contractionary fiscal policy). Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.3 mwezi Disemba 2018. Sarafu ya shilingi ukilinganisha na dola ya Kimarekani ilikuwa na utulivu na ilisimama kwa kiwango cha shilingi 2,281.20 kwa dola moja ya kimarekani.

Utekelezaji wa Mikakati kwa mwaka 2018

Ikichangiwa na kuimalika kwa msingi wa mazingira ya ki-uchumi na hali ya utulivu wa kisiasa nchini, DSE imefanikiwa kutekeleza baadhi ya shughuli za kimkakati zilizoanishwa katika Mpango Mkakati wa Miaka Mitano. Mipango hiyo ni pamoja na: i.) kuorodhesha dhamana nne (TCCIA na NICOL katika sehemu ya dhamana za hisa) na Kampuni ya TMRC na Benki ya NMB (katika soko la dhamana za Hatifungani); ii.) kuorodhesha hati fungani za serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 2,107; iii.) Kuongeza Wanachama wapya wawili wa Soko katika eneo la biashara ya hatifungani (Bonds Dealers); iv.) Kuimarisha uendeshaji wa kampuni tanzu ya CSDR; v.) DSE ilipata Uanachama kamili wa Shirikisho la Masoko ya Fedha Duniani (World Federation of Exchanges -WFE); na CSDR ilipata Uanachama kamili wa Chama cha Watunza Dhamana wa Afrika na Mashariki ya Kati (Africa & Middle East Depository Association -AMEDA); vi.) kuimarisha miundombinu ya uuzani, ununuzi na uhifadhi wa dhamana; na vii.) Kushiriki katika juhudi za kuanzishwa na kuorodhesha Hatifungani za Serikali za Mitaa.

Utawala Bora na Kuimarisha Ushirikiano Kimataifa

Kama sehemu ya kuzingatia na kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (UN Sustainable Development Goals), hasa Malengo manne (4) ambayo ni muhimu zaidi kwa Masoko ya Hisa, katika nyanja ya uwekezaji endelevu: Lengo Na. 5 - Kufikia Usawa wa Jinsia; Lengo Na.12 –Utumiajii na Uzalishaji Endelevu; Lengo Na. 3 - Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi; na Lengo Na.17 - Ushirikiano wa Maendeleo Endelevu

Ujumbe wa Mwenyekiti wa Bodi (inaendelea)

Utawala Bora na Kuimarisha Ushirikiano Kimataifa (inaendelea)

Duniani. DSE kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la “Global Compact” tualiandaa Warsha ya Gongga Kengele (Ring the Bell) kwa Usawa wa Jinsia, kama hatua za kutambua umuhimu wa usawa wa kijinsia katika maamuzi na uendeshaji wa biashara, kama sehemu ya utekelezaji wa lengo namba tano (5).

DSE ikiwa ni mshirika wa juhudi endelevu za Jumuiya ya Masoko ya Hisa Endelevu (UN-Sustainable Stock Exchanges) katika kuongoza shughuli za utekelezaji wa matakwa ya wawekezaji wenye mguso zaidi na mambo ya Mazingira, Jamii na Utawala Bora (Environmental, Social and Corporate Governance -ESG) kama moja ya mambo ya msingi ili kuwa na biashara endelevu. Ni katika muktadha huo na malengo hayo ya UN Sustainable Stock Exchanges, mwaka 2018 DSE ilifanya baadhi mipango kwa lengo la kuleta mwamko zaidi wa wanachama wake ikiwa ni pamoja na makampuni yaliorodheshwa juu ya masuala ya ESG. DSE iliyaweka masuala ya ESG katika tuzo zake za mwaka za Uanachama yaani DSE’s Annual Members Award (DMA). Lengo ni kuhakikisha makampuni yaliyorodheshwa katika soko la hisa na Madalali wa Soko wanakuwa na mwamko na kuzingatia matakwa ya sasa kimataifa katika uendeshaji wa shughuli za masoko ya hisa.

Katika utendaji wa kifedha, mwaka wa 2018 DSE ilipata Faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 1.8, wakati Rasilimali (Assets) zilikua kwa asilimia 1.9 na kufikia shilingi bilioni 19.5. Taarifa ya Afisa Mtendaji Mkuu itatoa mwangaza zaidi juu ya utendaji wa Kampuni kwa kipindi kinachoishia Disemba 2018.

Mikakati Muhimu kwa Mwaka 2019

Mwaka wa fedha wa 2019 utakuwa mwaka wa pili katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2018-2022). Mwaka 2019 mikakati muhimu ni pamoja na: Kufanya marekebisha ya Kanuni za DSE (DSE Rules) kwa lengo la kuongeza ufanisi wa soko na ukwasi; Kupanua wigo wa soko kwa njia ya kuongeza bidhaa na huduma mpya; kuhamasisha bidhaa mpya ambazo ni mahususi kwa wawekezaji wa rejareja, kama vile mifuko ya uwekezaji wa pamoja (Collective Investment Schemes CIS) na dhamana za reja reja; kupanga programu ambayo kwa ufanisi itawasidia wafanyabiashara wadogo na wakati kupata mitaji, kuongeza jitihada katika kuhakikisha DSE inatapatia utambuzi wa hadhi ya kuwa “Frontier Market” –(Frontier Market Status -FMS) na kuongeza udhibiti na usimamizi wa hatari na kuhakikisha Wanahisa wa DSE wanapatia rejesho la uwekezaji wa mtaji wa asilimia 15 (15 percent of Return on Equity).

Hitimisho na Mwelekeo

Kwa kuzingatia nafasi asilia katika sekta fedha, DSE inabakia kuwa kuwa kiunganishi muhimu kwa nchi na uchumi wa dunia. Kwa upande mwingine, hatari za athari hasi za uchumi wa dunia ikiwa ni pamoja na sera sizotabirika za nchi kubwa na hali ya kisiasa na misugvano ya kibiashara miongoni mwa mataifa makubwa, inawezekano wa kuathiri shughuli za biashara ya DSE; hii ikiwa ni pamoja na kutokuwa na uhakika wa matokeo ya vita vya kibiashara kati ya nchi za China na Marekani na Kujitoka kwa nchi ya Uingereza katika Jumuiya ya Ulaya. Hata hivyo, Mwelekeo chanya wa DSE kwa mwaka 2019 unajengwa na: i.) Ukuaji wa uwezo wa uchumi wa Tanzania; ii.) Uimara na uwazi wa soko la fedha za kigeni; iii.) Mwenendo wa misingi wa viendashaji uchumi (macro-economic performance); iv.) kuendelea kwa uwekezaji mkubwa katika miundombinu; na (v.) uimara wa hali ya siasa.

Ujumbe wa Mwenyekiti wa Bodi (inaendelea)

Hitimisho na Mwelekeo (inaendelea)

Sambamba na dhamira ya Serikali ya kuleta maendeleo ya huduma za ki-jamii na ki-uchumi kupitia sekta ya viwanda, DSE ina nafasi ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu kwa ajili ya miradi ya viwanda na miundombinu. Nina imani kubwa kwamba mpango mkakati wetu mpya utatuwezesha kukabiliana na ushindani utakaojitokeza katika mazingira haya uendeshaji. DSE tutaendelea kuwa katika mstari wa mbele katika kuzieleza sera nzuri za serikali zitakazosaidia kuleta makampuni mapya sokoni na kupanua wigo wa huduma na bidhaa za masoko ya mitaji nchini kwa mujibu wa Mpango wa Taifa ya Mfumo wa Fedha Jumuishi – (National Financial Inclusion Framework), 2018-2022. Mazingira wezeshi ya biashara yanayowekwa kwa pamoja na vyombo na taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na sekta binafsi, nina imani DSE tutaweza kujenga uwezo zaidi juu ya mafanikio tuliyopata katika mwaka 2018 na kufikia malengo yetu mapya na ukuaji wetu kwa miaka inayokuja.



Mwenyekiti wa bodi

Tarehe: 18/04/2019

WAKURUGENZI WA BODI



Bw. Jonathan Andrew Njau
Mwenyekiti



Bw. Joseph Mwisemba
Mjumbe wa Bodi



Bw. Andulile Mwakalyelye
Mjumbe wa Bodi



Bw. Wilhelm Ngasamiaku
Mjumbe wa Bodi



Bw. Riyaz Takim
Mjumbe wa Bodi



Bw. Ramadhan Unguu
Mjumbe wa Bodi



Bw. Moremi Marwa
Mjumbe wa Bodi
Afisa Mtendaji Mkuu



Bi. Mary Mniwasa
Katibu wa Bodi

Ujumbe wa Afisa Mtendaji Mkuu

Utangulizi

Mwaka wa 2018 ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mpango wetu wa miaka mitano - 2018 hadi 2022. Katika mwaka 2018 kampuni imepata matokeo mchanganyiko baina ya suala la utekelezaji wa mipango ya kimkakati, shughuli zilizopangwa kwa mwaka kwa upande mmoja na matokeo ya utendaji wa kifedha kwa upande wa pili.

Kwa upande wa utendaji wa soko, mwaka wa 2018 ulikuwa na changamoto katika nyanja ya ukwasi sokoni, kwa maana ya thamani ya mauzo na manunuzi ya hisa. Thamani ya mauzo hisa sokoini ilipungua kwa asilimia 60 kutoka shilingi bilioni 517 mwaka 2017 hadi kufikia mauzo ya shilingi bilioni 210 mwaka 2018. Hata hivyo, katika kipindi hicho kiasi cha idadi ya hisa zilizouzwa na kununuliwa kiliongezeka kwa asilimia 205, kutoka hisa milioni 290 zilizouzwa mwaka 2017 hadi kufikia hisa milioni 790 mwaka 2018.

Kushuka kwa thamani ya mauzo ya hisa kuliathiri mapato yetu, miamala ya mauzo na manunuzi ya hisa ilichangia asilimia 17 ya mapato yetu yote katika mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 33 mwaka 2017.

Kwa sehemu ya soko la hatifungani (fixed income segment), biashara katika soko la upili iliongezeka kwa asilimia 24, kutoka mauzo ya hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 859 mwaka 2017 hadi shilingi bilioni 1,063 mwaka 2018. Kwa upande wa Faharisi za soko, Faharisi zote yaani ile ya hisa zote (DSEI) na mtaji wa soko (market capitalization) zilipungua kwa asilimia 15. DSEI ilipungua kutoka pointi 2,396.32 pointi ya Desemba 31, 2017 hadi pointi 2,041.39 tarehe 31 Desemba 2018. Kwa muhtadha huo huo, Faharisi ya kampuni za ndani yaani "Tanzania Share Index -TSI" na ukubwa wa soko kwa kampuni za ndani yaani "Domestic Market Capitalization" zilipungua kwa asilimia 6: TSI kutoka pointi 3,919.25 Desemba mwaka 2017 hadi pointi 3,691.36 Desemba 2018, na ukubwa wa mtaji wa soko kwa kampuni za ndani ulishuka kutoka shilingi bilioni 10,275 mwaka 2017 hadi Shilingi bilioni 9,696 mwaka 2018, sababu kubwa ya kupungua kwa Faharisi hizi, ni kushuka kwa thamani za hisa za kampuni zinazounda Faharisi hizi.

Utendaji wa Kampuni ya DSE kwa Pamoja na Kampuni Tanzu (Group Performance)

Kama ilivyokwisha elezwa hapo awali, kushuka kwa kiwango cha shughuli za mauzo ya hisa katika mwaka 2018 kulichangia kwa kiwango kikubwa kupungua kwa mapato katika mwaka huu. Jumla ya mapato ilipungua kutoka mapato ya shilingi bilioni 10.70 kwa miezi 18 ya mwaka 2016/17 hadi kufikia shilingi bilioni 6.43 kwa miezi 12 ya mwaka 2018. Mwaka wa fedha 2017 ulikuwa ni wa miezi 18 miezi kufuatia mabadiliko wa mzunguko wa mwaka fedha kwa DSE kutoka Julai/June na kuwa Januari/Disemba kuanzia hapo mwaka 2016, wakati takwimu za mwaka 2018 ni za kipindi cha kawaida cha miezi 12 ya mwaka. Pamoja na hali hiyo ya kushuka kwa utendaji wa kifedha katika mwaka 2018, DSE bado ina uhakika wa kuendelea kuwa katika nafasi nzuri ya kutoa faida bora kwa wanahisa wake.

Utekelezaji wa Mkakati wa Kampuni

Kampuni ya DSE kwa ujumla (Group Company) inajiaminisha kwa Wadau wake na jamii pana tunayo ihudumia kuendelea kuzalisha na kukuza thamani ya uwekezaji wao. Tunaendelea kubaki imara katika kutoa thamani kwa wanahisa wetu kupitia yetu mikakati mbalimbali iliyoongozwa na misingi mitatu ya: Ubunifu, Ufanisi na Ufanikio.

Ujumbe wa Afisa Mtendaji Mkuu (inaendelea)

Mafanikio ya Mwaka 2018

Mpango mkakati kwa mwaka 2018 ulilenga katika kutekeleza na kufanikisha mambo mahimu yafuatayo: i.) Kuimarisha muundo wa shughuli za uendeshaji kwa DSE na CSDR; ii.) Kujishirikisha na watunga Sera katika shughuli za maendeleo ya sera na sheria za masoko ya mitaji; iii.) kufanya kazi na wadau mbalimbali katika uanzishwaji wa Hatifungani za Serikali za Mitaa pamoja na “M-Akiba Bond”; iv.) kuimarisha ukwasi wa soko, kupitia Miundombinu ya soko pamoja na muonekano wake; v.) kuimarisha mfumo wa kisheria na udhibiti kwa CSDR; (vi) kuhamia kwenye jingo jipya la ofisi lililopo katika mradi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC Morocco Square Project); vii.) Kupata Uanachama wa Kamili katika Shirikisho la Masoko ya Hisa Duniani (World Federation of Exchanges -WFE) na katika Shirikisho la Watunza Hifadhi za Dhamana wa Nchi za Afrika na Mashariki ya Kati (Africa & Middle East Depository Association -AMEDA); viii.) kuboresha ufanisi katika matumizi ya rasilimali za kampuni; na ix.) Kuimarisha mifumo ya miundombinu ya DSE & CSDR (mfumo wa huduma ya usajiri (registry system) Pamoja mifumo ya uendeshaji katika ofisi za Madalali wa Soko (Brokers Back Office System -BBO); x.) kuongeza uimara katika shughuli za udhibiti, kufuata taratibu na sharia zilizopo (compliance) na mifumo ya udhibiti athari (Risk Management Systems).

Tunayo furaha kutoa taarifa kwamba utekelezaji wa mikakati hii kwa mwaka 2018, umefanikiwa kwa asilimia 80.

Mwelekeo Kwa Mwaka 2019

Katika mwaka 2019 DSE itaendelea na shughuli za utekelezaji wa mpango mkakati wa miaka mitato 2018-2022 ambayo unalenga kuifanya DSE kuwa “Soko la Dhamana linalo changia katika kujenga uchumi kupitia utoaji wa bidhaa na huduma zake mbalimbali kwa bei nafuu na inayovutia watumiaji wake”

Katika mwaka 2019, mikakati ya Kampuni itajikita katika maeneo muhimu yafuatayo: (i) Kumaliza marekebisho ya Kanuni za Uendeshaji Soko (DSE Rules); (ii) Kubuni na kutekeleza taratibu za kukuza ukwasi wa soko kufikia uwiano wa angalau asilimia 5 ya thamani ya mitaji kwa kampuni za ndani (Domestic Market Capitalization) na angalau asilimia 10% ya thamani ya Hatifungani za Serikali; (iii) Kuongeza wigo wa huduma za soko, tukilenga shughuli za ukubwa wa soko kuwa angalau asilimia 20 ya Pato la Taifa (Market Cap to GDP ratio) kwa kuendeleza au kuongeza thamani ya ukubwa wa soko kupitia ongezeko la idadi ya kampuni sokoni na thamani ya dhamana moja moja ziliorodheshwa -kuorodhesha angalau dhamana mpya mbili, kuorodhesha hati fungani mbili za mashirika; kuorodhesha dhamana moja ya Serikali za Mitaa; (iv) kuorodhesha kampuni moja ya ETFs na kuorodhesha mfuko wa uwekezaji wa pamoja (Collective Investment Schemes - CIS) zinazo walenga wawekezaji wa reja reja; (v) kushiriki shughuli za mabadiliko ya Sera zinazohusu masoko ya hisa; kushirikiana na wadau wengine katika kuorodhesha dhamana ya Serikali za Mitaa; (vi) Kuanzisha programu inayolenga kujenga uwezo wa kampuni za saizi ya kati kuweza kutumia huduma za masoko ya hisa “DSE Enterprise Incubation / Acceleration Programu”; (vii) Kuongeza muonekano wa DSE kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na mitandao ya kijamii, uandishi wa Makala; (viii) kuboresha tovuti ya DSE; (ix) kuendesha shindano la uwekezaji kwa wanafunzi (DSE SIC) na Shindano la Wanachama wa DSE (DSE Members Award). Kuendeleza jitihada kwa lengo la kufikia hadhi ya kuwa “Frontier” Market Status”; (x) Kuzingatia kuimarisha DSE udhibiti wa shughuli za uendeshaji, kufuata taratibu, kanuni na sharia zinazoendesha soko na udhibiti wa athari mbalimbali kiendeshaji; na (xi) kuongeza ufanisi wa shughuli DSE na kusababisha kukuza faida; Kuhakikisha Kuzingatia.

| Ujumbe wa Afisa Mtendaji Mkuu (inaendelea)

Mwelekeo Kwa Mwaka 2019 (inaendelea)

PFMI / IOSCO viwango / misingi ya FMIs; Kukuza biashara ya Huduma za Usajili kwa kulenga wateja wa DSE na CSDR.

Shukurani

Napenda kuwashukuru wadau wetu wote kwa ushirikiano mzuri na usioyumba, waliotupatia katika mwaka 2018 tukiendelea kufanya kazi kwa bidii katika kujenga kampuni imara na yenye mafanikio zaidi wakati ujao. Tunapoingia mwaka 2019, napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu DSE kuwa kuufanya mwaka 2018 kuwa wa mafanikio na tukiangalia mambo yaliyo mbele safari yetu.

Napenda kuwashukuru wanahisa wetu wote kwa ushirikiano na uaminifu wao kwa Menejimenti ya DSE. Napenda kwa dhati kabisa kuwashukuru Bodi ya Wakurugenzi ya DSE kwa uongozi wao imara na muongozo waliotupatia katika mwaka 2018. Natarajia ushauri wenu na busara katika awamu ya nyingine ya ukuaji wetu. Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, Serikali na taasisi zake, hasa Mamlaka ya Masoko ya Hisa na Dhamana (CMSA) kwa kuweka mazingira mazuri ya usimamizi wa shughuli za uendeshaji soko, hali iliyopelekea DSE kufikia mafanikio iliyofikia katika mwaka huu.



Moremi Marwa

Mtendaji Mkuu.

Tarehe: 18/04/2019

MENEJIMENTI



Bw. Moremi Marwa
Afisa Mtendaji Mkuu



Bw. Ibrahim Mshindo
Mkurugenzi wa Maendeleo
ya Biashara



Bi. Mary Miwasa
Mwanasheria wa Kampuni



Bw. Emmanuel Nyalali
Meneja Kazi Maalum
Ofisi ya Afisa Mtendaji Mkuu



Bw. Ali Othman
Asifa Mkuu wa Teknolojia



Bw. Mecklaud Edson
Mkaguzi Mkuu wa Ndani



Bw. Benitho Kyando
Mtendaji Mkuu wa Kampuni
Tanzu (CSDR)



Bw. Lucas Sinkala
Meneja wa Fedha

Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi

1. UTANGULIZI

Bodi ya Wakurugenzi wa Dar es Salaam Stock Exchange PLC (“DSE”) na furaha kuwasilisha ripoti yake pamoja na taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2018 inayoeleza hali halisi ya DSE na kampuni yake tanzu, CSDR (kwa pamoja hujulikana kuwa “kundi la kampuni”) katika tarehe hiyo.

2. USAJILI

Dar es salaam Stock Exchange PLC (iliyokuwa inajulikana kwa jina la Dar es salaam Stock Exchange Limited) ilisajiliwa mwaka 1996 kwa sheria ya kampuni ya Tanzania, 2002 (yaani Companies Act) kuwa kampuni ya dhima yenye kikomo kwa dhamana (company limited by Guarantee), shughuli za DSE zilianza Aprili 1998. Tarehe 26 Juni 2015, kampuni ilibadili usajili wake kutoka hadhi ya kampuni yenye dhima ya dhamana na kuwa kampuni inayomilikiwa na wanahisa (kampuni ya umma yenye kikomo) na hatimaye kubadili jina lake kutoka Dar es salaam Stock Exchange Limited kuwa Dar es salaam Stock Exchange PLC na kutoa hisa ishirini za TZS 400 kila moja. Mwezi Juni 2016, DSE iliua hisa kwa umma katika soko la awali na baadaye kuorodhesha hisa zake kwenye soko la hisa tarehe 12 Julai 2016.

3. DIRA

Kuwa injini inayosukuma shughuli za uchumi kwa kuwezesha upatikanaji mitaji kwa ajili ya miradi ya kiuchumi na hivyo kuwa chachu ya taifa ya mabadiliko kuelekea hadhi ya kuwa “Frontier Market Status” (FMS) kwa kushawishi upatikanaji wa mtaji na uwekezaji.

4. DHAMIRA

Kukuza utajiri wa wanahisa/wamiliki wa DSE kwa kutumia rasilimali za kampuni na pia kubuni uwezeshaji wa kiuchumi kwa kuwezesha ufanisi katika upatikanaji mitaji.

5. SHUGHULI KUU

Shughuli kuu ya DSE ni kuwa soko la dhamana kwa wawekezaji wanaokusudia kuwekeza kwenye kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa linalotoa jukwaa linalosaidia kampuni kuongeza mtaji kupitia uzaji wa hisa na dhamana, DSE pia imeanzisha kampuni tanzu inayomilikiwa kwa ukamilifu iitwayo CSD Registry Company Limited (CSDR) ambayo shughuli zake kuu ni kutunza kumbukumbu ya miamala iliyofanywa katika DSE na kuhakikisha malipo na uhamishwaji wa umiliki unafanyika kama inavyoelekezwa na Sheria na Kanuni za soko la hisa.

6. UTENDAJI WA FEDHA

Faida kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2018 ilikuwa TZS 1,757,688,000 – (kwa mwaka wenye miezi 12) na mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2017: TZS 5,266,462,000 (mwaka wenye miezi 18 kufuatia mabadiliko ya mzunguko wa mwaka wa fedha kuanzia mwaka Julai mwaka 2016) .

Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi (inaendelea)

7. UTAWALA WA KAMPUNI

Wajumbe wote wa Bodi isipokuwa Afisa Mtendaji Mkuu, si watendaji. Wakurugenzi wanazingatia misingi ya utawala bora wa kampuni, na kutambua umuhimu wa kufanya biashara kwa kuzingatia mwenendo bora unaokubalika kwa kufanya hivyo, wakurugenzi kwa hiyo wanathibitisha kuwa:

- i. Bodi imekutana kama kawaida katika kipindi chote cha taarifa hii.
- ii. Bodi ina udhibiti kamili na wenye ufanisi wa kampuni na hufuatilia menejimenti kuhusu utendaji wa kampuni.
- iii. Nafasi za Mwenyekiti wa Bodi na Afisa Mtendaji Mkuu (CEO) zinashikwa na watu wawili tofauti.
- iv. Bodi inakutana na kufanya maamuzi ya kimkakati na kisera na pia kuidhinisha bajeti na kufuatilia utendaji.

8. BODI YA WAKURUGENZI YA DSE

Bodi ya wakurugenzi iliyokuwa madarakani katika kipindi chote mpaka tarehe ya ripoti hii ni:

Jina	Nafasi	Sifa	Taifa	Umri	Tarehe ya kuteuliwa	Tarehe ya kujiuzulu
Bi. J.K.Ndissi	Si Mkurugenzi Mtendaji	BA & MA Economics	Mtanzania	64	2015	Januari 2018
Bw. J. Njau	Si Mkurugenzi Mtendaji	LLB & MBA - Finance	Mtanzania	57	Septemba 2016	29 Januari 2019
Bw.E. Busara	Si Mkurugenzi Mtendaji	MBA. CPA (T)	Mtanzania	45	Septemba 2016	9 Februari 2018
Bw.R. Takim	Si Mkurugenzi Mtendaji	BSC & MSC Economics	Mtanzania	45	Septemba 2016	17 Septemba 2018
Bw.U. Sulay	Si Mkurugenzi Mtendaji	MSC Accounting & Finance, FCCA and ACPA	Mtanzania	42	31 Julai 2017	3 Januari 2019
Bw.J. Mwaitemba	Si Mkurugenzi Mtendaji	MBA. CPA (T)	Mtanzania	38	13 Octoba 2017	2 Januari 2019
Bw.V. Shah	Si Mkurugenzi Mtendaji	B.Sc. in Electronics and Computer Science, MBA in IT Management	Mtanzania	52	12th Juni 2018	7 Januari 2019
Bw.F. Manongi	Si Mkurugenzi Mtendaji	B.Arts (hons.) in Economics and Finance, Master of Arts in Development Economics	Mtanzania	64	22nd Septemba 2018	31 Disemba 2018
Bw.A. Mwakalyelye	Si Mkurugenzi Mtendaji	M.A Economics	Mtanzania	59	Aprili 2017	28 Agosti 2018
Dk. W. Ngasamiaku	Si Mkurugenzi Mtendaji	Phd. Economics	Mtanzania	44	31 Julai 2017	-
Bw.M. Marwa	Mkurugenzi Mtendaji.	MBA, CPA (T)	Mtanzania	42	2015	-

Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi (inaendelea)

9. MALIPO YA WAKURUGENZI

Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE) imelipa jumla ya TZS 143,223,856 Kwa ada ya wakurugenzi (Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2017: TZS 97,517,900).

10. MIKUTANO NA SHUGHULI ZA BODI

a) Bodi alikutana 8 katika kipindi cha Januari 2018 hadi Desemba 31, 2018 kama ifuatavyo

Jina	8 Feb 2018	14 Mar 2018	18 Mei 2018	29 Juni 2018	18 Aug 2018	23 Aug 2018	15 Nov 2018	11 Des 2018
Bw.J. Njau	√	√	√	√	√	√	√	√
Bw.R. Takim	-	-	√	-	√	√	N/A	N/A
Bw.A. Mwakalyelye	√	√	√	√	√	√	N/A	N/A
Dk. W. Ngasamiaku	√	√	-	√	√	√	√	√
Bw.E. Busara	√	N/A	N/A	N/A	N/A	N/A	N/A	N/A
Bw.U. Sulay	√	√	√	√	√	√	√	√
Bw.J. Mwaisemba	√	-	√	√	√	√	-	-
Bw.V. Shah	N/A	N/A	N/A	N/A	N/A	N/A	√	√
Bw.F. Manongi	N/A	N/A	N/A	N/A	N/A	N/A	√	√
Bw.M. Marwa	√	√	√	√	√	√	√	-

Bodi ilijadili na kuamua mambo yaliyopendekezwa na kamati za kudumu na ilitoa maagizo kwa menejimenti kuhusu masuala ya uendeshaji. Bodi inasaidiwa na kamati zifuatazo kama ilivyokuwa Desemba 31 2018.

(b) Kamati ya Kuorodhesha na Usimamizi wa Miamala/Biashara
(Listing and Tradwing Committee -LTC)

Jina	Cheo	Sifa	Taifa
Bw.Jonathan Njau	Mwenyekiti	LLB & MBA – Finance	Tanzanian
Bw.Wilhelm Ngasamiaku	Mjumbe	Phd. Economics	Tanzanian
Bw.Andulile Mwakalyelye	Mjumbe	BSC & MSC ADMIS	Tanzanian

Kamati ya Kuorodhesha na Usimamizi wa Miamala/ Biashara (LTC) inaripoti kwa bodi ya DSE. Kamati hii imekutana mara tisa (9) katika kipindi cha taarifa hii. Kamati imejadili maombi mbalimbali kwa ajili ya kuorodheshwa kwa kampuni na dhamana katika soko.

Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi (inaendelea)

10. MIKUTANO NA SHUGHULI ZA BODI (INAENDELEA)

(c) Kamati ya uongozi na udhibiti wa Athari (Administrative, Risk and Compliance -ARC).

Jina	Cheo	Sifa	Taifa
Bw.R. Takim	Mwenyekiti	BSC & MSC ADMIS	Mtanzania
Bw.A. Mwakalyelye	Mjumbe	MA Economics	Mtanzania
Bi. J. K. Ndissi	Mjumbe	BA & MA Economics	Mtanzania

Kamati ya Usimamizi na udhibiti wa Athari (ARC) inaripoti kwa Bodi ya DSE. Kamati hii imekutana mara nne (4) kujadili masuala mbalimbali ya mambo ya wafanyakazi, mambo ya kitendaji na usimamizi na maombi ya wanachama washiriki wapya.

d) Audit Committee

Jina	Cheo	Sifa	Taifa
Bw.U. Sulay	Mwenyekiti	MSC Accounting & Finance and FCPA	Mtanzania
Bw.R. Takim	Mjumbe	BSC & MSC ADMIS	Mtanzania
Bw.E. Busara	Mjumbe	MBA. CPA (T)	Mtanzania
Bw.J. Mwisemba	Mjumbe	MBA. CPA (T)	Mtanzania

Kamati ya Ukaguzi wa mahesabu inaripoti kwa Bodi ya DSE. Kamati hii imekutana mara nne (4) katika kipindi cha taarifa hii kujadili mambo mbalimbali kama vile ripoti za fedha za robo mwaka za DSE, Ripoti za ukaguzi wa ndani na ukaguzi wa nje wa DSE kwa kupindi kilichoishia tarehe 31 Desemba 2018.

11. MENEJIMENTI

Menejimenti ya DSE iko chini ya Afisa Mtendaji Mkuu na imepangwa katika idara zifuatazo:

- Idara ya Fedha na Utafiti,
- Idara ya Sheria na Usimamizi wa Taratibu
- Idara Miradi na Uendelezaji Biashara
- Idara ya Data za Soko na Biashara.
- Idara ya TEHAMA.
- Idara ya mkaguzi wa ndani.

12. KUWEZA KULIPA

Bodi ya wakurugenzi ya DSE inathibitisha kwamba viwango vya utunzaji hesabu fedha vinavyotumika vimefuatwa na kwamba taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia mahitaji ya kampuni yenye mlengo endelevu (going concern). Wajumbe wa Bodi wana maoni kuwa DSE ina uwezo wa kulipa madeni yake kulingana na maana iliyodhaniwa na Sheria ya kampuni Tanzania, mwaka 2002.

Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi (inaendelea)

13. VIDOKEZO MUHIMU VYA KIPINDI CHA TAARIFA

Wakati wa kipindi cha taarifa hii utendaji wa uendeshaji wa soko la hisa ulikuwa kama ulivyooneshwa hapa chini.

Maelezo	Mwaka unaoishia 31 December 2018	Kipindi cha miezi 18 kinachoishia 31 December 2017
Mtaji wa soko (TZS- Bilioni)	19,677	23,076
Mtaji wa soko la ndani (TZS- Bilioni)	9,696	10,226
Thamani ya Hisa zilizouzwa (TZS – Bilioni)	208	711
Thamani ya hatifungani zilizouzwa (TZS – Bilioni)	969	889
Pointi za faharasa za hisa zote (DSEI)	2,041	2,396
Pointi za Faharasa za hisa za Tanzania (TSI)	3,691	3,919
Thamani ya hatifungani zilizo rodheshwa na kubaki (TZS Bilioni)	9,436	8,108

14. UPEO WA BIASHARA

DSE ni soko la hisa lililoidhinishwa rasmi chini ya sheria ya Masoko ya Mtaji na Dhamana ya 1994 (SURA YA 79). Ni soko la hisa la kisasa linalouza dhamana kwa kutumia mifumo ya kieletroniki, kupitisha na kulipa dhamana (hisa na hatifungani). Pia DSE ni mamlaka inayojiendesha (SRO) juu ya wanachama wake kwa madhumuni ya kulinda uadilifu wa soko.

15. UPEO WA RIPOTI

Ripoti ya mwaka kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 December 2018 kinaonesha seti ya ripoti za mwaka na taarifa za fedha kwa kipindi kilichoanzia tarehe 01 January 2018 mpaka tarehe 31 December 2018. Taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya utoaji Taarifa za Fedha ya Kimataifa (IFRS) na zaidi ya hapo, imefuata masharti ya Sheria ya Kampuni ya 2002.

16. MUUNDO WA MTAJI

DSE ilisajiliwa tarehe 19 Septemba mwaka 1996 kama kampuni ya dhima yenye kikomo kwa dhamana bila mtaji wa hisa. Soko la hisa lilianzishwa kushughulikia pamoja na mambo mengine, kuwezesha utekelezaji wa sera za mageuzi ya kiuchumi, kubinafsisha mashirika ya serikali na kuiwezesha sekta binafsi kupata mitaji ya muda mrefu. DSE ilianza kufanya kazi rasmi April 1998. Mnamo tarehe 29 Julai 2015, DSE ilibadili hadhi yake kutoka kampuni ya dhima yenye kikomo kwa njia ya dhamana na kuwa kampuni ya dhima yenye kikomo kwa njia ya hisa na jina lake kuwa Dar es salaam Stock Exchange PLC. DSE iliuzwa hisa zake kwa umma na tarehe 12 Julai 2016 ilijiorodhesha kwenye soko la hisa.

Muundo wa kuimiliki hisa wa DSE kama ilivyokuwa tarehe 31st December 2018 kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi (inaendelea)

16. MUUNDO WA MTAJI (INAENDELEA)

Na	Mwanahisa	Idadi ya hisa	Asilimia ya hisa zinazomilikiwa
1	Serikali ya Tanzania (kupitia, msajili wa hazina – TR)	3,574,000	15%
2	SCB (T) NOMINEES SCB - Consumer Banking Re Bw.Aunali F. Rajabali and Sajjad F. Rajabali	2,984,624	13%
3	SCB (T) NOMINEE RE SCB Mauritius A/C Briarwood Chase Management LLC A/C Briarwood Capital Partners LP	2,848,314	12%
4	National Investment Company Limited	1,285,831	5%
5	Wanahisa wengine	13,131,231	55%
	Total	23,824,000	100%

17. UDHIBITI WA MASHAKA NA UDHIBITI WA NDANI

Bodi ya wakurugenzi inabeba jukumu la mwisho kuhusiana na mifumo ya udhibiti wa athari hasi na udhibiti jumla wa soko la Hisa. Ni wajibu wa menejimenti kuhakikisha kuwa mifumo ya ndani ya udhibiti wa uendeshaji na udhibiti wa fedha inafanya kazi sawa na matarajio na kwamba mahesabu ya kifedha na vitabu vya mahesabu ya fedha inatayarishwa na kuendeshwa kwa kuzingatia Taratibu za kampuni endelevu ili kutoa uhakika unaofaa kuhusu:

- Kufaa kwa ufanisi wa uendeshaji.
- Kulinda rasilimali za soko la hisa.
- Kufuata sheria na kanuni zinazotakiwa.
- Kuaminika kwa kumbukumbu za utunzaji hesabu za fedha.
- Uendelevu wa biashara katika hali ya kawaida au hali mbaya.
- Tabia na mwenendo inayofaa kwa wadau wote.

Ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani wowote hutegemea zaidi ufuataji kwa dhati wa hatua zilizoлезwa. Daima kuna hatari ya kutofuata hatua hizo na watumishi. Mfumo wa soko la hisa umetayarishwa ili kuipatia bodi uhakika unaofaa na kwamba taratibu zilizopo zinafanyakazi kwa ufanisi.

Bodi ilitathmini mifumo ya udhibiti wa ndani katika kipindi chote cha taarifa ya fedha kilichoishia tarehe 31 Disemba 2018 na inaona kuwa imetimiza vigezo vinavyokubalika. Bodi inafanya tathmini ya udhibiti wa ndani na mashaka. Kupitia kamati ya usimamizi na udhibiti na kamati ya ukaguzi.

18. KURUDISHA FADHILA KWA JAMII

DSE imetimiza jukumu lake kwa jamii katika kipindi cha taarifa hii. Jumla ya TZS 11 million (December 2017: TZS 0.15 million) zilichangiwa kwa bunge la Jamhuri wa Tanzania, ili kuwezesha ujenzi wa vyoo kwa ajili ya wanafunzi wa kike.

Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi (inaendelea)

18. KURUDISHA FADHILA KWA JAMII (INAENDELEA)

DSE pia imewawezesha wanafunzi kutoka taasisi za elimu ya juu kujifunza jinsi ya kuwekeza rasilimali pesa kwa kutumia data halisi na mfumo wa kufanyia biashara (ATS) na hivyo kuwezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo kuhusu namna ya kuweka akiba na kuwekeza kupitia soko la hisa. Hii ilitekelezwa kama sehemu ya kampeni ya elimu kwa umma kupitia programu ya changamoto za uwekezaji kwa wanafunzi (yaani DSE Scholar Investment Challenge).

19. USTAWI WA WATUMISHI

Afya na matibabu

DSE inatoa bima ya matibabu kwa watumishi na familia zao kupitia huduma za matibabu ya kampuni ya AAR Insurance (T) Limited. Huu ni mkataba wa mwaka mmoja unaoweza kuongezwa. Katiba kipindi cha taarifa hii, huduma zilizotolewa na mtoa huduma zilikuwa zinaridhisha kwa jumla.

Idadi ya watumishi

Hadi tarehe 31st December 2018, DSE ilikuwa na watumishi 19 miongoni mwao 8 walikuwa wanawake na 11 wanaume. Mwaka 2017 kulikuwa na jumla ya watumishi 21 miongoni mwao 8 walikuwa wanawake na 13 wanaume.

20. WAKAGUZI

Pricewater House Coopers wameonesha utayari wao wa kuendelea kufanya kazi na DSE kwa mujibu wa kifungu cha 170 (2) cha sheria ya kampuni ya mwaka 2002 (Sura ya 212). Uteuzi wa wakaguzi kwa mwaka unaoishia tarehe 31 December 2019 utafanywa katika mkutano mkuu wa mwaka..

KWA MAMLAKA YA BODI


Imeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 18/04/2019 na kutiwa saini kwa naiba ya Bodi na:



Dk. W. Ngasamiaku

18/04/2019

Tarehe



Bw.M. Marwa

18/04/2019

Tarehe


Taarifa Ya Bodi Ya Wakurugenzi (inaendelea)

Sheria ya Kampuni Na. 12 ya Mwaka 2002 (Sura ya 212) inawataka wakurugenzi, watayarishaji taarifa za fedha kwa kila mwaka wa fedha zinazotoa maoni ya kweli na yasiyo na upendeleo kuhusu hali halisi ya kampuni katika mwisho wa mwaka wa fedha na faida au hasara, kwa kila mwaka. Pia inawataka wakurugenzi wahakikishe kuwa kampuni zinatunza kumbukumbu za utunzaji wa fedha zinazoonesha, kwa usahihi wa kutosha, hali ya fedha ya Kampuni. Pia wana wajibu wa kulinda mali / rasilimali za kampuni na hivyo kuchukua hatua zinazostahili za kuzuia na kubaini udanganyifu, kughushi, kosa na ukiukaji mwingine wa sheria..

Wakurugenzi wanakubali jukumu kwa taarifa za fedha zilizotayarishwa kwa kutumia sera za utunzaji fedha zinazostahili ziambatanazo na uamuzi wa busara na makadirio kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji taarifa za fedha (IFRS) na masharti ya sheria ya kampuni Na. 12 ya mwaka 2002 (Sura ya 212). Wakurugenzi wanatoa taarifa za fedha zinazoonesha maoni ya kweli na yasiyo na upendeleo kuhusu mambo ya fedha ya kundi la kampuni na faida yake kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya utoaji Taarifa za fedha (IFRS). Pia wakurugenzi wanakubali wajibu kwa utunzaji wa kumbukumbu za hesabu za fedha zinazoweza kuaminiwa katika matayarisho na uwasilishaji usio na upendeleo wa taarifa za fedha zisizo na upotoshaji iwe kutokana na udanganyifu, kughushi au kosa.

Hakuna ambacho wakurugenzi wamekiona kuashiria kuwa kampuni itashindwa kuwa endelevu (going concern) kwa angalau miezi 12 kuanzia tarehe ya taarifa hii.

Imetiwa sainsi kwa niaba ya bodi ya wakurugenzi na



Dkr. W. Ngasamiaku

18/04/2019

Tarehe



Bw.M. Marwa

18/04/2019

Tarehe

A MB'S PAMOJA
KAZA ZIADAI

1

2



50

RELAX WITH
NEED'S





FOMU YA UWAKILISHI



DAR ES SALAAM STOCK EXCHANGE PLC

Katibu wa Kampuni
Dar es Salaam Stock Exchange PLC
S.L.P 70081
Dar Es Salaam

Tafadhali jaza kwa herufi kubwa

Mimi/Sisi wa S.L.P,
..... nikiwa mwanahisa/tukiwa wanahisa wa Dar es Salaam Stock
Exchange PLC, namchagua / tunamchagua wa
S.L.P, kuwa mwakili/wawakilishi wangu/wetu na kupiga
kura kwa niaba yangu/yetu katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kampuni utakaofanyika siku ya
Jumanne tarehe 25 Juni 2019, Hoteli ya New Africa, Dar Es Salaam au mahali popote patakapoamuliwa.

Saini yangu/zetu zimeshuhudiwa leo tarehe 2019.

.....
(Saini)



DAR ES SALAAM STOCK EXCHANGE PLC

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA NNE WA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Nne wa Wanahisa wa Kampuni ya Soko la Hisa la Dar Es Salaam utakaofanyika Hoteli ya New Africa iliyopo kona ya Mtaa wa Azikiwe na barabara ya Sokoine Dar Es Salaam, siku ya Jumanne tarehe 25 Juni 2019 kuanzia sa tatu na nusu asubuhi (9.30 a.m.) kwa madhumuni yafuatayo:

1. Kupisha ajenda ya mkutano;
2. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Tatu wa Mwaka;
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Tatu wa Mwaka;
4. Kupokea na kupitisha
 - 1.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya DSE kwa Mwaka uliyoishia tarehe 31 Disemba, 2018;
 - 1.2 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya DSE na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2018;
 - 1.3 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya *Fidelity Fund* na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2018;
5. Kupitisha Malipo ya Wakaguzi wa Nje;
6. Uteuzi wa Wakaguzi wa Nje kwa Mwaka wa Fedha 2019;
7. Kuidhinisha Malipo ya Ada ya Wakurugenzi kwa Mwaka wa Fedha 2019;
8. Kuidhinisha Malipo ya Gawio kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2018;
9. Kuchagua Wajumbe Wapya wa Bodi ya Wakurugenzi ya DSE; na
10. Mengineyo.

Maelezo

1. Mwanahisa atakaye hudhuria mkutano atatakiwa kufika na nakala ya *Depository Receipt* pamoja na kitambulisho chake.
2. Vitabu vyenye taarifa za hesabu kwa mwaka 2018 pamoja na fomu ya mwakilishi vitapatikana katika Ofisi za DSE, Ghorofa ya 3, Jengo la Kambarage, Mtaa wa Ufukoni na kwa Madalali wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam kuanzia Jumatatu tarehe 10 Juni 2019.
3. Mwanahisa yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano ana haki ya kuchagua mwakilishi au wawakilishi na kupiga kura kwa niaba yake. Endapo mwanahisa ni shirika, mwakilishi anatakiwa kuwa na fomu za uwakilishi ziwe zimegongwa muhuri wa kampuni. Fomu hizo zifikishwe kwa Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi katika ofisi za DSE kabla ya saa nane mchana (02:00 p.m.) Jumatatu tarehe 24 Juni 2019.
4. Orodha (Register) ya Wanahisa watakaostahili kupiga kura itafungwa Jumatatu tarehe 19 Juni 2019.

Kwa Agizo la Bodi

Mary Stephen Mniwasa
Katibu wa Bodi
4 Juni 2019